

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**  
**IMETHIBITISHWA NA ISO 9001:2015**



**UAMUZI NA.6 WA GHARAMA ZA MWINGILIANO WA MITANDAO YA WATOA HUDUMA  
ZA MAWASILIANO YA SIMU KATIKA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA,  
UMETOLEWA JULAI, 2023.**

## **1.0 UTANGULIZI**

Uamuzi huu umefanywa chini ya Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, Sura ya 172 ya Sheria za Tanzania (Ikirejewa kama Sheria ya TCRA). Kwa kuzingatia matakwa ya Kifungu cha 18(2) (b) na 18 (5) cha Sheria ya TCRA, 2003, Jopo la Uchunguzi lilifanya uchunguzi wa gharama za mwingiliano wa mitandao kuanzia tarehe 13 hadi 26 Juni, 2023 ili kupata maoni kutoka kwa wadau. Jopo la Uchunguzi lilizingatia pamoja na mambo mengine, ripoti ya utafiti wa gharama za kutoa huduma za mawasiliano nchini, uliofanywa na kampuni ya ushauri ya *M/S Incyte Consulting Ltd.* Utafiti ulitumia njia mseto ya kukokotoa gharama za mwingiliano (Hybrid Long Run Incremental Cost Study Methodology-LRIC+).

Uamuzi huu utajulikana kama Uamuzi Na.6 uliotolewa mwaka 2023 kuhusu gharama za mwingiliano wa mitandao ya watoa huduma za mawasiliano nchini (hapa inajulikana kama "Uamuzi"). Uamuzi huu utaanza kutumika kuanzia tarehe Januari Mosi, 2023 na utatumiwa na watoa huduma za mawasiliano katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

## **2.0 MATOKEO YA JOPO LA UCHUNGUZI**

Baada ya kupitia kwa kina ripoti ya uchunguzi wa gharama za mwingiliano wa mitandao, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) inakubaliana na mapendekezo ya Jopo la Uchunguzi wa gharama ambalo lililoteuliwa kwa mujibu wa Kanuni ya 6(1) ya TCRA (*Procedure for Rules of Inquiry*) Rules, 2004. Notisi ya Uchunguzi ilichapishwa katika Gazeti la Serikali kama Tangazo la Serikali Na.395A tarehe 13 Juni 2023. Notisi hiyo pia ilichapishwa katika magazeti ya kila siku ambayo ni gazeti la *Daily News*, Mwananchi na Habari Leo tarehe 14 Juni 2023. Notisi ya Uchunguzi ilitolewa kwa watoa huduma za mawasiliano nchini pamoja na wadau wengine waliotajwa kwenye Notisi ya Uchunguzi.

Uchunguzi ulifanyika kwa kuzingatia takwa la utoaji wa uamuzi wa gharama za mwingiliano kulingana na Kifungu cha 18(2) (b) na 18 (5) cha Sheria ya TCRA. Mchakato wa uchunguzi ulihusisha mapitio ya nyaraka mbalimbali, mashauriano, maoni kutoka kwa wadau na umma kwa ujumla. Hatimaye, Jopo la Uchunguzi lilitoa ripoti ambayo iliwasilishwa kwa Bodi ya TCRA tarehe 26 Juni, 2023.

Mamlaka inakubaliana na maoni ya Jopo la Uchunguzi kwamba kila mtoa huduma anaukiritimba katika huduma za simu zinazoishia kwenye mtandao wake. Ili kukuza ushindani katika soko, kuna umuhimu wa Mthibiti kuingilia kati na kuelekeza kuhusu gharama za mwingiliano wa mitandao. Pia, TCRA inakubaliana na pendekezo la kupunguza gharama za mwingiliano wa mitandao ya simu lililowasilishwa na Jopo.

TCRA imeridhika kwamba, Jopo la Uchunguzi liliridhishwa na njia iliyotumika katika kufanya utafiti wa gharama za mwingiliano wa mitandao ya simu, na kuwa njia hiyo ndiyo msingi katika kubainisha gharama za mwingiliano kwa sababu inazingatia gharama halisi za sasa na zijazo, kupitia mtoa huduma mwenye kutumia teknolojia ya kisasa kwa ufanisi (*Modern Efficient Operator-MEO*).

Wadau walikuwa na maoni tofauti kuhusu viwango vya gharama za mwingiliano zilizopendekezwa, wengine walipendekeza kuwa viwango viwe juu kwa hoja kwamba kiwango cha juu cha gharama za mwingiliano kinahitajika ili kuvutia uwekezaji na kudumisha uendeleu wa kipato. Wengine walipendekeza viwango viwe chini zaidi ili kuwezesha huduma za mawasiliano ya simu zinapatikane kwa bei nafuu zaidi kwa wateja.

### 3.0 UAMUZI

Kwa kuzingatia maelezo hapo juu, TCRA inatoa maamuzi yafuatayo:

- 3.1 Inaelekeza kuwa viwango vya juu za gharama za mwingiliano ya mitandao ya watoa huduma za mawasiliano za simu kwa miaka mitano ijayo kama zilivyooneshwa kwenye Jedwali 1.

#### **Jedwali 1: Gharama za mwingiliano (TZS/Dakika) kuanzia Januari Mosi, 2023 hadi 31 Disemba 2027:**

Mwaka	Januari Mosi, 2023	Januari Mosi, 2024	Januari Mosi, 2025	Januari Mosi, 2026	Januari Mosi, 2027
Gharama za mwingiliano wa mitandao kwa dakika	1.86	1.76	1.68	1.60	1.52

- 3.2 Gharama za mwingiliano zitahusisha simu zote za ndani zinazoishia katika mitandao ya watoa huduma za mawasiliano katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
- 3.3 Watoa huduma za mawasiliano wako huru kujadiliana, kukubaliana na kutumia gharama za mwingiliano ambazo ni za chini kuliko zile zilizotolewa kupitia uamuzi huu;
- 3.4 Watoa huduma za mawasiliano wanatakiwa kuingia mikataba mipya ya gharama za mwingiliano wa mitandao ya simu na kuwasilisha nakala za mikataba hiyo TCRA kabla ya tarehe 31 Julai, 2023.

Dkt. Jabiri K. Bakari  
**MKURUGENZI MKUU**  
**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**